

➤ **UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA KATA YA KEZA JANUARI 2018.**

Uchaguzi mdogo katika kata ya Keza jimbo la Ngara ulitokana na nafasi kuwa wazi kwasababu ya kifo cha Diwani wa kata ya keza kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi(CCM) kilichotokea tarehe 03/08/2017.

Kwa mujibu wa Masharti ya kifungu cha 13(3) cha sharia za uchaguzi wa serikali za mitaa(madiwani) sura 292,Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza uwepo wa nafasi wazi ya Udiwani na kujazwa kwa kufanyika uchaguzi mdogo uliofanyika tarehe 13/01/2018.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliwateuwa watumishi 6 wa Halmashauri ya wilaya ya Ngara kuwa wasimamizi wa Uchaguzi mdogo wa Udiwani katika kata ya Keza kwa mtiririko ufuatao;-

1. Aidan J.Bahama - Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo (RO).
2. Jmary I.Abdul - Afisa Uchaguzi (w) (EO)
3. Kalwa A.Mombo - Msimamizi Msaidizi wa Jimbo (ARO)
4. Burilo M.Deya - Msimamizi Msaidizi wa Jimbo (ARO)
5. Josephine J.Lusatira – Msimamizi Msaidizi wa Kata (ARO-KATA)
6. Yotham John - Msimamizi Msaidizi wa Kata (ARO-KATA)

Pamoja na Uteuzi huu Wateule wote walikula Kiapo cha Kutunza Siri na cha Kujitua Uanachama wa Chama Chochote cha Siasa kama wana vyama mbele ya Hakimku Mkazi wa Mkoa wa Dodoma tarehe 07/12/2017.

Vyama vya Siasa vilivyojitokeza na kuleta barua za utambulisho kutoka katika vyama vyao ili kuweza kuchukua fomu za uteuzi kwa nafasi ya Udiwani kata ya Keza na kuteuliwa kugombea Udiwani ni kama ifuatavyo:-

1. CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) – Bw. Bakundukize Valesi Gwaibondo.
2. NCCR-Mageuzi - Bw. Eradius Emmanuel Bitemele.
3. The Civil United Front (CUF) - Bw. Philpo Joseph Bazubwenge.

SIKU YA UCHAGUZI

Uchaguzi ulifanyika tarehe 13/01/2018, vituo vilifunguliwa mapema saa 1:00 asubuhi vituo vyote vilianza kupiga kura. Vituo vilifungwa saa 10:00 jioni na kura zilihesabiwa vituoni hadi saa 12 jioni vituo vyote viliwasilisha matokeo Makao Makuu ya Kata ili kujumlishwa.

- Waliotarajiwa Kupiga Kura Ni 4,109
- Waliopiga kura 1153 (28%)
- Kura halali 1,127
- Kura zilizoharibika 26.

Ushiriki wa Upigaji kura kwa kila kituo ni kama ifuatavyo:-

| NA | JINA LA KITUO | WALIOANDIKISHWA | WALIOPIGA KURA | KURA HALALI | ZILIZOHA RIBIKA |
|-----|----------------------------|-----------------|----------------|-------------|-----------------|
| 1. | NYANZA CENTRE 1 | 361 | 103 | 97 | 06 |
| 2. | NYANZA CENTRE 2 | 361 | 105 | 104 | 01 |
| 3. | SHULE YA MSINGI GWENZAZA 1 | 323 | 42 | 41 | 01 |
| 4. | SHULE YA MSINGI GWENZAZA 2 | 326 | 50 | 49 | 01 |
| 5. | SHULE YA MSINGI KIBIRIZI 1 | 303 | 98 | 97 | 01 |
| 6. | SHULE YA MSINGI KIBIRIZI 2 | 302 | 113 | 108 | 05 |
| 7. | SHULE YA MSINGI RUKILA 1 | 379 | 102 | 99 | 03 |
| 8. | SHULE YA MSINGI RUKILA 2 | 380 | 100 | 100 | 00 |
| 9. | SHULE YA SEKONDARI KEZA 1 | 258 | 57 | 57 | 00 |
| 10. | SHULE YA SEKONDARI KEZA 2 | 258 | 65 | 65 | 00 |
| 11. | SHULE YA MSINGI KEZA 1 | 431 | 164 | 162 | 02 |
| 12. | SHULE YA MSINGI KEZA 2 | 430 | 154 | 148 | 06 |
| | JUMLA | 4109 | 1153 | 1127 | 26 |

MATOKEO YA KURA KWA WAGOMBEA

| Na. | JINA KAMILI | CHAMA | IDADI YA KURA ALIZOPATA | % | MAONI |
|-----|--------------------------|----------------|-------------------------|-------|---------------------|
| 1. | Bakundukize V. Gwaibondo | CCM | 1,019 | 88.38 | Alitangazwa mshindi |
| 2. | Philpo J. Bazubwenge | CUF | 73 | 6.3 | |
| 3. | Eradius E. Bitemele | NCCR - MAGEUZI | 35 | 4.59 | |
| | JUMLA | | 1,127 | | |

MATUMIZI YA FEDHA ZA UCHAGUZI MDOGO KATIKA KATA YA KEZA

Jumla ya **Tshs 31,334,000/=** zilipokelewa kutoka TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI (NEC) kwa ajili ya shughuli za uchaguzi mdogo wa Udiwani katika kata ya Keza na zilitumika kwa mujibu wa Mwongozo wa matumizi ya Fedha kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Aidha, Matumizi yote yamezingatia Sheria za malipo na mwongozo ikiweo Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011.

Changamoto.

Pamoja na usimamizi mzuri, idadi kubwa ya wapiga kura haikujitokeza kwa sababu mbalimbali zikiweo. Siku ya Jumamosi ni siku ya Soko - Rulenge - Wananchi wengi hushiriki shughuli za soko

- Umbali mrefu wa wapiga kura

- Hali ya hewa na msimu wa kilimo.
- Kwa upande wa uendeshaji, Fedha kidogo kwa ajili ya gharama zingine kwa walinzi wa doria na uendeshaji semina.